# Samia atema nyongo

Na Gabriel Mushi

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameibua sakata la vikwazo vya kibiashara vilivyokuwepo kati ya Serikali ya Kenya na Tanzania huku akikumbushia tukio la kuteketezwa kwa moto kwa shehena ya vifaranga vya kuku kutoka Kenya.

Rais Samia alisema mzozo huo wa ki- biashara kati ya Tanzania na Kenya uliotokea wakati wa Serikali ya awamu ya tano, ulisababisha mvutano usio na maana, lakini tangu alipoingia madarakani pande hizo mbili zilikutana na kumaliza tofauti zilizokuwepo.

"Tulikuwa tunavutana hapa na Kenya kila kinachokwenda hakipiti, huku hakipiti na kule hakipiti, kule wakizuia na mkuu wa mkoa wetu anasema hakipiti, lakini tulikaa tukaelezana ukweli.

"Tulikuwa tunachomeana kuku mipakani, dhambi tupu... viumbe wa Mungu mnamwagia petroli mnawachoma, haikuwa na maana! Lakini tumeondosha vikwazo sasa biashara imekuwa mno. Ukiangalia figure za biashara Kenya na Tanzania imekuwa mno," alisema Rais Samia.

Rais Samia alitoa kauli hiyo jana mbele ya Rais wa Uganda, Yoweri Museven katika Kongamano la Biashara kati Tanzania na Uganda, huku akisisitiza kuwa anataka biashara kati ya nchi hizo mbili ikue zaidi.

Katika kipindi cha awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, serikali zaidi ya mara mbili iliteketeza kwa moto vifaranga vya kuku kutoka Kenya.

Mara ya kwanza iliteketeza vifaranga 6,700 na mara ya pili vifaranga zaidi ya 5,000 vilivyodaiwa kuingizwa nchini kupitia mpaka wa Namanga kutoka Kenya.

Sababu kadhaa za kuchukua hatua hiyo zilitolewa, ikiwamo taarifa kwamba vifaranga hao walingizwa bila kibali, huku mamlaka zikidai kuwa wanaweza kueneza homa ya mafua ya ndege.

Hatua hiyo iliyoshutumiwa na wanaharakti wa wanyama kutoka mataifa yote mawili, lakini pia ilisababisha vita vya kibiashara kati ya mataifa hayo jirani na hata kuzuia ndege za nchi moja kuingia nchi nyingine.



Rais Samia Suluhu Hassan.

Akiwa ziarani mkoani Kagera mwaka 2018, Rais Magufuli alizungumzia sababu za kuteketeza viumbe hao, akisema serikali yake itaendelea kukamata mifugo watakaoingia nchini kutoka taifa jirani kwani, Tanzani sio shamba la kuchungia mifugo ya nchi jirani.

Pia alizitaka nchi jirani kuchukua hatua kama hiyo iwapo mifugo ya Tanzania itaingia nchini mwao kinyume na sheria.

Mbali ya kufukua sakata la kuteketezwa kwa moto kwa vifaranga hao, Rais Samia alimshukia Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda aliyeapa kutokutoa vibali vya kununua sukari kutoka nje ya nchi.

Rais Samia alimhakikishia Rais Museven kwamba Tanzania itanunua sukari kutoka nchini humo huku akikosoa kwa ukali kauli ya Waziri Mkenda.

Kauli ya Rais Samia imekuja ikiwa imepita miezi miwili tangu Prof. Mkenda aliposema yuko tayari kuachia ngazi nafasi ya uwaziri kuliko kutoa kibali kwa wafanyabiashara kuagiza sukari kutoka nje ya nchi.

Agosti 30, 2021, wakati akizindua ripoti ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa Kilimo 2019/2020 jijini Dodoma, Prof. Mkenda alisema kumekuwa na shinikizo kutoka kwa wafanyabiashara wanaokwenda kuisumbua Bodi ya Sukari kutaka kibali cha kuagiza sukari nje ya nchi.

"Unajua sukari ni kama dawa za kulevya, ina hela nyingi na kila mtu anataka kufanya biashara hiyo. Kuna mawaziri wa kilimo wameondoka kwa sababu ya kutoa vibali vya sukari. Mimi sitoi ng'o," alisema Prof. Mkenda.



Makasha yenye vifaranga

Rais Samia ambaye juzi alimpokea Rais Museveni aliyewasili nchini kwa ziara ya siku tatu, alisema Uganda iliiomba Tanzania inunue sukari ya nchi hiyo.

"Rais Museveni amesema hapa aliomba sisi tununue sukari kwake, lakini walisikia statement za waziri wetu, kwamba hatutanunua, hatutakubali. That was non-sense, Rais Museveni tutanunua sukari kutoka Uganda," alisema Rais Samia.

Pamoja na mambo mengine alisisitiza mawaziri wa kisekta kutoka Uganda na Tanzania wakutane haraka kuangalia vikwazo vya kibiashara vilivyopo kati ya pande hizo mbili.

**BOMBA LA GESI**

Pia Rais Samia akizungumzia juu ya mradi wa bomba la mafuta na gesi kati ya Tanzania na Uganda alisema tayari Tanzania imeboresha mazingira ya uwekezaji kwa namna mbalimbali.

"Nafarijika kusema jitihada tulizochukua kwa kipindi kifupi cha takribani miezi nane, zimeleta chachu ya kuongezeka uwekezaji na idadi ya ajira zinazotarajiwa kutokana na miradi iliyoandikishwa.

"Tuendelee kukuza uwekezaji katika nyanja mbalimbali ikiwemo viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na viwanda vinavyotumia nguvu kazi zaidi ili kuongeza ajira, pamoja na viwanda vinavyozalisha viwanda vingine kama vya mbolea na kemikali.

"Tumefanya marekebisho ya sheria ya kuratibu ajira za wageni, ambapo kwa sasa sheria inaruhusu mwekezaji kuingiza wataalam hadi 10 kutoka idadi ya watano iliyokuwa kabla Oktoba 2021.

"Maboresho yamewezesha kupungua kwa muda wa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa kuondoa urasimu na sasa hata ndani ya siku moja mwombaji anaweza kupata kibali kupitia mfumo wa E-Permit. Mfumo huu pia unaruhusu upatikanaji kibali cha ukaazi katika kadi moja," alisema.

Kwa upande wake, Rais Museveni alisema tatizo kubwa la nchi za Afrika ni masoko bidhaa zinazotokana na rasilimali asili za nchi husika.

Alisema nchi hizo zimejaaliwa kuwa na rasilimali asili nyingi ambazo hazijatumika ipasavyo.

Alisema kuwa na rasilimali nyingi sio lazima nchi iwe tajiri kwa sababu hata Uganda wanazo nyingi ila siyo matajiri kwa sababu hazijatumiwa ipasavyo.

Scanned with CamScanner

